

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

**BARAZA LA USHAURI LA WATUMIAJI WA HUDUMA ZA
NISHATI NA MAJI (EWURA CCC)**



**MAONI YA BARAZA LA USHAURI LA WATUMIAJI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI
(EWURA CCC) JUU YA OMBI LA MAMLAKA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA
KASULU UWSA LA KUTAKA KUPANDISHA BEI ZA HUDUMA ZA MAJI KWA KIPINDI
CHA MIAKA MITANO KUANZIA 2026/27-2030/31**

1. Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA Consumer Consultative Council – EWURA CCC) linapenda kuwasilisha maoni yake kuhusu ombi la Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kasulu (Kasulu UWSA) la kuidhinishiwa mapitio ya bei za huduma za maji kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka wa fedha.

Maoni haya yametokana na mapitio ya nyaraka mbalimbali zilizowasilishwa na Kasulu UWSA pamoja ikiwemo:

- i. Maombi ya Mapitio ya Bei (Tariff Application),
 - ii. Mpango Biashara (Business Plan)
 - iii. Muhtasari wa Kikao cha Wadau (Stakeholder Consultation Minutes),
 - iv. Azimio la Bodi, Bajeti ya Mamlaka ya mwaka wa fedha 2025/26,
 - v. Taarifa za Fedha zilizokaguliwa kwa mwaka wa fedha 2024/25,
 - vi. Taarifa ya Mdhambi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG Report)
 - vii. Barua ya Wizara ya Maji ya kutotoa pingamizi (No Objection Letter),
 - viii. Kanuni za EWURA.
2. Baada ya kufanya mapitio hayo, Baraza limebaini kuwa Taarifa za fedha zilizokaguliwa kwa kipindi cha miaka mitatu iliyotangulia na Taarifa ya Utafiti kuhusu

utayari wa watumiaji kulipia bei mpya (Willingness to Pay Study) haikuambatishwa na maombi haya kinyume na Kanuni za EWURA.

Baraza linaamini kuwa, ukamilifu wa nyaraka za maombi si hitaji la kiutaratibu pekee bali ni msingi muhimu wa kuhakikisha kuwa mapitio ya bei yanafanyika kwa uwazi, uwajibikaji na kwa kuzingatia maslahi ya watumiaji. Nyaraka kama Mpango Biashara na taarifa za fedha za miaka iliyopita, ndizo zinazoonyesha uhalali wa uwekezaji unaopendekezwa, uhalisia wa makadirio ya gharama pamoja na maboresho ya huduma yanayotarajiwa kutokana na ongezeko la bei. Pale nyaraka hizo zinapokosekana au kutokuthibitishwa, uwezo wa EWURA na wadau, ikiwemo Baraza, kujiridhisha kuwa watumiaji hawatabebeshwa gharama zisizo na msingi hupungua.

Baraza linaishauri EWURA kuhakikisha kuwa kabla ya kufanya uamuzi wa mwisho kuhusu maombi haya, ithibitishwe ukamilifu wa nyaraka zote zinazotakiwa chini ya Kanuni ya 4 ya Kanuni za EWURA za Mwaka 2024, ili uamuzi utakaofanywa ujengwe juu ya taarifa kamili, sahihi na zinazolinda maslahi ya watumiaji wa huduma.

3. Nyaraka za Mamlaka yaani Mpango Biashara wa Mamlaka Maombi ya mapitio ya bei hazijaonesha uchambuzi wa kina kuhusu uwezo wa watumiaji kumudu gharama za huduma (Affordability Analysis) baada ya kutekelezwa kwa tariff mpya. Aidha, hakuna uchambuzi unaohusisha uwezo wa kaya za eneo la huduma kumudu viwango vinavyopendekezwa kwa kuzingatia hali yao ya kiuchumi, kipato au matumizi ya kawaida ya maji.

Aidha, Baraza limebaini kuwa, katika kikao cha wadau baadhi ya washiriki walionesha wasiwasi kuhusu kiwango cha ongezeko la bei na uwezo wa wananchi kukimudu. Hata hivyo, nyaraka zilizowasilishwa hazioneshi uchambuzi unaoeleza namna maoni hayo yalivyotumika kutathmini uwezo wa watumiaji kumudu bei mpya inayopendekezwa. Hali hiyo inapunguza uwezo wa kujiridhisha kuwa kiwango cha bei kinachopendekezwa kinaendana na hali halisi ya kiuchumi ya wananchi wanaohudumiwa na Kasulu WSSA.

Baraza linaona kuwa, uchambuzi wa uwezo wa watumiaji kumudu gharama za huduma ni sehemu muhimu ya mchakato wa mapitio ya bei kwa kuwa unasaidia kuhakikisha kuwa beimpya inafikia uwiano kati ya uendeleu wa Mamlaka na haki ya wananchi kupata huduma ya maji kwa gharama zinazomudu.

Baraza linashauri EWURA kuitaka Kasulu WSSA kuwasilisha uchambuzi wa kina kuhusu uwezo wa wananchi kumudu gharama mpya za huduma unayozingatia hali ya kiuchumi ya watumiaji na makundi mbalimbali ya wateja kabla ya kufanya uamuzi wa mwisho kuhusu maombi ya bei mpya zinazopendekezwa.

4. Uchambuzi wa nyaraka za Mamlaka umebaini kuwa Mamlaka ilifanya mashauriano na wadau kuhusu mapendekezo ya bei pamoja na kushirikisha wadau katika maandalizi ya Mpango Biashara. Hata hivyo, Baraza halikuona ushahidi katika nyaraka zilizowasilishwa unaoonesha kuwa kulifanyika Utafiti kuhusu Utayari wa Watumiaji kulipia kiwango cha bei mpya zinazopendekezwa.

Baraza linaamini, ushirikishwaji wa wadau katika mikutano ya mashauriano ni hatua muhimu ya kisheria na kiutawala, lakini peke yake hauwezi kuchukua nafasi ya uchambuzi wa kitaalamu unaopima uwezo na utayari wa watumiaji kulipia huduma baada ya ongezeko la bei. Utafiti wa aina hiyo husaidia kubaini kiwango ambacho watumiaji wanaweza kukikubali bila kuathiri upatikanaji wa huduma, pamoja na kutoa msingi wa kufanya uwiano kati ya uendeleu wa Mamlaka na maslahi ya watumiaji.

Aidha, kumbukumbu za kikao cha wadau zinaonesha kuwa baadhi ya washiriki walitoa maoni na hoja kuhusu mapitio ya bei yaliyopendekezwa. Hali hiyo inaonesha umuhimu wa kuwa na ushahidi wa ziada wa kitaalamu unaoonesha jinsi maoni na matarajio ya watumiaji yalivyozingatiwa katika kuandaa kiwango cha tariff kilichowasilishwa kwa EWURA.

Baraza linashauri EWURA kuhakikisha kuwa maombi ya mapitio ya bei yanaungwa mkono na ushahidi wa kutosha kuhusu utayari wa watumiaji kulipia huduma (*Willingness to Pay*), au uchambuzi mwingine unaolingana na lengo hilo, ili kuwezesha

kufanya uamuzi unaozingatia kwa uwiano uendelevu wa Mamlaka na uwezo wa watumiaji kumudu gharama za huduma.

5. Mamlaka imeeleza mipango ya kuongeza kiwango cha huduma ya maji kutoka asilimia 71 hadi asilimia 95, kupanua mtandao wa usambazaji na kuongeza idadi ya wateja wanaopata huduma. Aidha, nyaraka zinaonesha kuwa miongoni mwa makundi ya wateja wanaohudumiwa na Kasulu WSSA ni watumiaji wa majumbani, taasisi, wafanyabiashara pamoja na watumiaji wa maji kupitia Kiosks.

Hata hivyo, Baraza halikuona uchambuzi mahsusi unaoonesha namna ambavyo Bei mpya inayopendekezwa itaathiri makundi yenye mazingira maalum ya kijamii na kiuchumi, hususan kaya zenye kipato cha chini, watumiaji wanaotegemea huduma yamaji kwenye Kiosks, shule, vituo vya kutolea huduma za afya pamoja na makundi mengine yanayoweza kuwa katika mazingira magumu. Vilevile, nyaraka hazioneshi kama kulifanyika tathmini ya iwapo makundi hayo yataendelea kumudu gharama za huduma baada ya utekelezaji wa tariff mpya.

Baraza linaona kuwa pamoja na umuhimu wa kuhakikisha uendelevu wa Mamlaka, mchakato wa mapitio ya bei unapaswa pia kuzingatia kanuni ya usawa katika upatikanaji wa huduma (equity in access to services). Maji ni huduma ya msingi ya kijamii na kiuchumi, hivyo ongezeko la bei linapaswa kuandamana na hatua zinazolinda makundi yenye uwezo mdogo wa kumudu gharama za huduma ili yasije yakapungua uwezo wa kupata huduma salama na endelevu.

Baraza linashauri EWURA kuhakikisha kuwa kabla ya kuidhinisha bei mpya ya huduma Mamlaka iwasilishe uchambuzi unaoonesha athari za bei mpya kwa makundi maalum ya watumiaji, hususan kaya zenye kipato cha chini, watumiaji wa maji kwenye Kiosks, shule, vituo vya kutolea huduma za afya na makundi mengine yaliyo katika mazingira magumu. Aidha, pale inapobainika kuwa makundi hayo yanaweza kuathiriwa kwa kiwango kikubwa, EWURA izingatie hatua stahiki za udhibiti zitakazolinda upatikanaji wa huduma kwa makundi hayo bila kuathiri uendelevu wa Mamlaka.

6. Baraza limepitia makadirio ya gharama za uendeshaji na matengenezo (O&M) pamoja na mahitaji ya mapato (Revenue Requirements) yaliyowasilishwa na Kasulu WSSA na kubaini ongezeko kubwa la gharama zinazopendekezwa kurejeshwa kupitia bei za huduma. Taarifa zilizopo kwenye Nyaraka ya Maombi ya Bei (Tariff Application) zinaonesha kuwa, jumla ya gharama za uendeshaji kabla ya uchakavu (depreciation) zinaongezeka kutoka takribani Shilingi bilioni 3.914 katika mwaka 2024/25 hadi Shilingi bilioni 17.521 katika mwaka 2025/26, na kufikia Shilingi bilioni 18.869 katika mwaka 2026/27. Aidha, mapato yanayohitajika kutokana na mauzo ya maji yanaongezeka kutoka takribani Shilingi bilioni 3.914 mwaka 2024/25 hadi Shilingi bilioni 17.673 mwaka 2025/26 na Shilingi bilioni 18.977 mwaka 2026/27 (Tariff Application, Fomu Na. 4 na 5, uk. 15–24).

Baraza limebaini kuwa ongezeko hilo halijaendana na taarifa za matumizi na mapato halisi zilizooneshwa katika Hesabu za Fedha Zilizokaguliwa. Taarifa hizo zinaonesha kuwa jumla ya matumizi ya Kasulu WSSA katika mwaka 2024/25 ilikuwa takribani Shilingi milioni 599.7, huku mapato kutokana na mauzo ya maji yakiwa takribani Shilingi milioni 509.23 na fedha zilizopokelewa kutokana na miamala ya kubadilishana zikiwa takribani Shilingi milioni 451.46 (CAG Report, Financial Statements and Notes, uk. 44–50). Hivyo, kuna tofauti kubwa kati ya gharama na mapato halisi yaliyokaguliwa na kiwango kilichowasilishwa kama msingi wa sasa wa makadirio ya gharama na Revenue Requirement.

Aidha, Baraza limebaini kuwa baadhi ya vipengele vikuu vya gharama vinaongezeka kwa kiwango kikubwa. Kwa mfano, gharama ya umeme kwa ajili ya uzalishaji wa maji inaongezeka kutoka Shilingi milioni 437.94 mwaka 2024/25 hadi takribani Shilingi bilioni 2.609 mwaka 2025/26, wakati gharama za kemikali zinaongezeka kutoka Shilingi bilioni 1.336 hadi takribani Shilingi bilioni 4.635 katika kipindi hicho (Tariff Application, Fomu Na. 4, uk. 15–16).

Kwa upande mwingine, Hesabu za Fedha Zilizokaguliwa zinaonesha matumizi halisi ya mwaka 2024/25 ya takribani Shilingi milioni 48.09 kwa umeme, Shilingi milioni 3.57

kwa kemikali za maji na Shilingi milioni 19.61 kwa vifaa vingine vya kemikali (CAG Report, Notes 21 na 23, uk. 45 na 49–50).

Gharama za watumishi zinaongezeka kutoka Shilingi milioni 751.69 mwaka 2024/25 hadi takribani Shilingi bilioni 1.845 mwaka 2025/26 na Shilingi bilioni 2.110 mwaka 2026/27, wakati matumizi halisi ya mishahara, ujira na mafao ya watumishi yaliyooneshwa katika Hesabu za Fedha Zilizokaguliwa kwa mwaka 2024/25 yalikuwa takribani Shilingi milioni 242.36 (Tariff Application, Fomu Na. 4, uk. 17–18; CAG Report, Note 19, uk. 44). Gharama za utawala nazo zinakadiriwa kuongezeka kutoka Shilingi milioni 762 mwaka 2024/25 hadi takribani Shilingi bilioni 6.167 mwaka 2025/26 (Tariff Application, Fomu Na. 4, uk. 18–23).

Baraza linatambua kuwa ongezeko la baadhi ya gharama linaweza kusababishwa na upanuzi wa huduma, kuanza kutumika kwa miundombinu mipya pamoja na mahitaji ya ziada ya uzalishaji na usambazaji wa maji. Hata hivyo, tofauti kubwa iliyopo kati ya matumizi yaliyokaguliwa na makadirio yaliyowasilishwa inahitaji maelezo ya kina yanayoonesha kiasi cha huduma kitakachoongezeka, tarehe za kuanza kutumika kwa miundombinu mipya, matumizi ya umeme, kiasi na bei za kemikali, mpango wa ajira pamoja na gharama nyingine zinazohusiana moja kwa moja na utoaji wa huduma.

Kwa msingi huo, Baraza linashauri EWURA kufanya tathmini ya kina ya uhalali wa gharama hizo (prudency review) kwa kulinganisha kila kipengele kikuu cha gharama katika Fomu Na. 4 na Hesabu za Fedha Zilizokaguliwa, Bajeti na shughuli zilizoainishwa katika Mpango wa Biashara. Kasulu WSSA itakiwe kuwasilisha mchanganuo unaoonesha kiasi, bei kwa kila kipimo, tarehe za utekelezaji na sababu za ongezeko la kila gharama. Gharama ambazo hazijathibitishwa, zimejirudia au hazihusiani moja kwa moja na utoaji wa huduma zisioongezwe katika Revenue Requirement itakayorejeshwa kupitia bei zinazolipwa na watumiaji.

7. Baraza limepitia taarifa za mali, uchakavu, ruzuku za Serikali pamoja na vyanzo vya fedha vinavyotarajiwa kugharamia shughuli na uwekezaji wa Kasulu WSSA. Kwa mujibu wa Fomu Na. 4 na 5, gharama ya depreciation inaongezeka kutoka takribani

Shilingi milioni 157.734 mwaka 2024/25 hadi Shilingi milioni 297.205 mwaka 2025/26, na kuendelea kuongezeka katika kipindi cha mapitio ya bei (Tariff Application, Fomu Na. 4 na 5, uk. 23–24). Hesabu za Fedha Zilizokaguliwa zinathibitisha depreciation ya Shilingi milioni 157.734 kwa mwaka 2024/25 na thamani ya kubeba ya mali, mitambo na vifaa ya takribani Shilingi bilioni 3.047 (CAG Report, Note 14, uk. 43).

Baraza limebaini kuwa kiwango cha uchakavu cha mwaka 2024/25 kilichooneshwa katika maombi kinaendana na taarifa zilizokaguliwa. Hata hivyo, ongezeko la depreciation katika miaka inayofuata halijaambatanishwa na mchanganuo wa kila mali unaoonesha aina na thamani ya mali, chanzo cha fedha, muda wa matumizi, tarehe inayotarajiwa kukamilika na tarehe ya kuanza kutumika. Bila taarifa hizo, ni vigumu kujiridhisha kuwa depreciation inayopendekezwa inahusu mali zinazostahili, zilizokamilika na zinazotumika moja kwa moja katika utoaji wa huduma.

Aidha, Hesabu za Fedha Zilizokaguliwa zinaonesha kuwa Kasulu WSSA ilipokea ruzuku ya Serikali ya takribani Shilingi milioni 827.025 katika mwaka 2024/25 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya mradi wa maji Kasulu (CAG Report, Note 18, uk. 44). Bajeti ya mwaka 2025/26 nayo inaonesha matarajio ya ruzuku za Serikali ya takribani Shilingi bilioni 6.423, ikilinganishwa na mapato ya ndani ya takribani Shilingi bilioni 2.118 (Annual Budget FY 2025/26, Budget Summary and Income Sources). Hata hivyo, Fomu Na. 5 inaonesha makato ya “other income” ya kati ya takribani Shilingi milioni 145 na Shilingi milioni 236 pekee katika kipindi cha tariff (Tariff Application, Fomu Na. 5, uk. 24).

Baraza linaona kuwa tofauti hiyo inahitaji ufafanuzi wa wazi kuhusu namna ruzuku za Serikali, fedha za wafadhili na vyanzo vingine visivyotokana na tariff zilivyotambuliwa katika Revenue Requirement. Endapo gharama za mali au miradi iliyofadhiliwa na Serikali au wafadhili zitajumuishwa tena katika depreciation, rate base au gharama za uwekezaji zinazorejeshwa kupitia bei, watumiaji wanaweza kulipia mara ya pili gharama ambazo tayari zimegharimiwa kupitia fedha za umma.

Vilevile, taarifa zilizokaguliwa zinaonesha Work in Progress ya takribani Shilingi milioni 426.815, lakini maombi hayaoneshi kwa uwazi miradi inayounda kiasi hicho, asilimia ya utekelezaji, chanzo cha fedha na tarehe inayotarajiwa ya kukamilika. Mali ambayo bado haijakamilika au haijaanza kutumika haipaswi kuanza kutozwa depreciation kana kwamba tayari inatoa huduma kwa watumiaji.

Kwa msingi huo, Baraza linashauri EWURA kuitaka Kasulu WSSA kuwasilisha Asset Register, mchanganuo wa depreciation kwa kila mali, orodha ya miradi iliyo chini ya utekelezaji pamoja na jedwali la vyanzo vya fedha kwa kila mradi. EWURA ijiridhishe kuhusu umiliki, chanzo cha fedha, thamani, muda wa matumizi na tarehe ya kuanza kutumika kwa kila mali kabla ya kuruhusu depreciation au gharama nyingine za mali kurejeshwa kupitia tariff. Aidha, ruzuku zote za Serikali na wafadhili zilinganishwe na miradi na Revenue Requirement, na gharama zilizofadhiliwa kupitia ruzuku zisioongezwe tena katika bei zinazolipwa na watumiaji, isipokuwa pale Kanuni zinaporuhusu wazi.

8. Baraza limepitia makadirio ya Mahitaji ya Mapato (Revenue Requirement) na mapato yanayotarajiwa kutokana na mauzo ya maji yaliyowasilishwa na Kasulu WSSA kwa kipindi cha mapitio ya bei. Fomu Na. 5 inaonesha kuwa mapato yanayotarajiwa kutokana na mauzo ya maji yataongezeka kutoka takribani Shilingi bilioni 3.914 mwaka 2024/25 hadi Shilingi bilioni 17.673 mwaka 2025/26 na kufikia takribani Shilingi bilioni 18.977 mwaka 2026/27 (Tariff Application, Form 5, uk. 24).

Hata hivyo, Baraza limebaini kuwa Hesabu za Fedha Zilizokaguliwa zinaonesha kuwa mapato halisi yaliyotokana na mauzo ya maji katika mwaka 2024/25 yalikuwa takribani Shilingi milioni 509.227, huku mapato yaliyopokelewa kutokana na miamala ya kubadilishana (cash receipts from exchange transactions) yakiwa takribani Shilingi milioni 451.458 (CAG Report, Note 17 na Budget Performance Statement, uk. 44 na 47).

Baraza linaona kuwa ongezeko kubwa la mapato yanayotarajiwa kutokana na mauzo ya maji linahitaji kuungwa mkono na ushahidi wa kutosha unaoonesha namna

yatakavyopatikana katika kipindi husika. Pamoja na kwamba Kasulu WSSA imeainisha mikakati ya kuboresha huduma, kupanua mtandao wa usambazaji, kuongeza wateja na kuboresha ukusanyaji wa mapato, maombi hayajaonesha kwa uwazi uhusiano kati ya ongezeko la idadi ya wateja, kiasi cha maji kitakachouzwa, uwezo wa uzalishaji, kiwango cha ukusanyaji wa mapato na kiwango cha mapato kinachotarajiwa kufikiwa kupitia tariff mpya.

Kwa mtazamo wa Baraza, makadirio ya Revenue Requirement yanapaswa kuzingatia si tu ongezeko la gharama bali pia uwezo halisi wa Mamlaka kuzalisha, kusambaza, kubili na kukusanya mapato yanayokadiriwa. Makadirio yasiyoendana na uwezo wa utekelezaji yanaweza kusababisha watumiaji kubebeshwa ongezeko la bei lisiloakisi uhalisia wa utoaji wa huduma au kusababisha Mamlaka kushindwa kufikia malengo ya mapato yaliyowekwa.

Kwa msingi huo, Baraza linashauri EWURA kuitaka Kasulu WSSA kuwasilisha uchambuzi wa kina unaunganisha Revenue Requirement na viashiria vya utekelezaji, ikiwemo ongezeko la wateja, kiasi cha maji kitakachozalishwa na kuuzwa, kiwango cha bili zitakazokusanywa, uwezo wa uzalishaji wa miundombinu pamoja na maboresho ya ufanisi yanayotarajiwa. EWURA ijiridhishe kuwa makadirio ya mapato yanayotokana na tariff mpya yanaweza kufikiwa kwa uhalisia kabla ya kuyatumia kama msingi wa kuidhinisha ongezeko la bei.

9. Viwango vya bei vinavyopendekezwa na Kasulu WSSA vinaonesha ongezeko kubwa la bei kwa makundi mbalimbali ya wateja. Kwa mfano, bei ya maji kwa wateja wa majumbani inapendekezwa kuongezeka kutoka Shilingi 300 hadi Shilingi 3,050 kwa mita ya ujazo, wakati kwa taasisi inapendekezwa kuongezeka kutoka Shilingi 400 hadi Shilingi 3,115 na kwa wateja wa biashara kutoka Shilingi 510 hadi Shilingi 3,420 kwa mita ya ujazo (Tariff Application, uk. 7 na 26).

Hata hivyo, pamoja na ukubwa wa ongezeko hilo, maombi hayajaambatanisha Bill Impact Analysis unaoonesha namna ongezeko la bei litakavyobadilisha bili za watumiaji kwa viwango tofauti vya matumizi ya maji, kwa mfano kaya zinazotumia

kiwango cha chini, cha wastani au kikubwa cha maji, pamoja na taasisi na wateja wa biashara. Kukosekana kwa uchambuzi huo kunafanya kuwa vigumu kutathmini athari halisi za tariff mpya kwa watumiaji wa kila kundi.

Kwa mtazamo wa Baraza, Bill Impact Analysis ni nyenzo muhimu inayomwezesha mdhibiti na wadau kuelewa kwa uwazi mabadiliko ya bili yatakayowakabili watumiaji baada ya kuidhinishwa kwa tariff mpya. Uchambuzi huo huongeza uwazi katika mchakato wa mapitio ya bei na husaidia kutathmini kama kiwango cha ongezeko kinawiana na maboresho yanayotarajiwa katika utoaji wa huduma.

Kwa msingi huo, Baraza linashauri EWURA kuitaka Kasulu WSSA kuwasilisha Bill Impact Analysis unaoonesha mabadiliko ya bili kwa viwango tofauti vya matumizi na kwa kila kundi la wateja, ili kuwezesha tathmini sahihi ya athari za tariff inayopendekezwa kabla ya kufanya uamuzi wa mwisho.

10. Mpango Biashara wa Kasulu WSSA umeweka malengo ya kuboresha utendaji wa Mamlaka katika maeneo muhimu ya utoaji wa huduma, ikiwemo kuongeza kiwango cha huduma ya maji, kuongeza muda wa upatikanaji wa huduma, kupunguza kiwango cha maji yanayopotea (Non-Revenue Water – NRW), kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato pamoja na kuimarisha huduma kwa wateja. Ili kufanikisha malengo hayo, Mamlaka imeandaa mpango wa utekelezaji unaojumuisha miradi ya kuongeza uzalishaji wa maji, upanuzi wa mtandao wa usambazaji, ufungaji wa mita za maji na bulk meters, kuongeza wateja wapya pamoja na hatua mbalimbali za kuboresha usimamizi wa huduma (Business Plan, uk. 1–2, 17–20 na 53–57).

Hata hivyo, Baraza limebaini kuwa tathmini ya utendaji wa sasa wa Kasulu WSSA bado inaonesha uwepo wa changamoto katika baadhi ya viashiria muhimu vya huduma. mfano kiwango cha huduma ya maji ni asilimia 71, wastani wa upatikanaji wa huduma ni saa 10.1 kwa siku, kiwango cha maji yasiyoingiza mapato ni asilimia 40 na ufanisi wa ukusanyaji wa mapato ni asilimia 76. Hali hiyo inaonesha kuwa bado kuna pengo kubwa kati ya hali ya sasa na malengo yaliyowekwa na Mamlaka kwa kipindi cha Mpango Biashara (Business Plan, uk. 11–12).

Kwa mtazamo wa Baraza, mafanikio ya mapitio ya bei hayapaswi kupimwa kwa kuongezeka kwa mapato ya Mamlaka pekee, bali pia kwa kiwango ambacho watumiaji watanufaika kupitia maboresho yanayoonekana katika utoaji wa huduma. Kwa kuwa sehemu ya gharama zinazopendekezwa kurejeshwa kupitia tariff inakusudiwa kufadhili utekelezaji wa shughuli hizo za maendeleo na maboresho ya huduma, ni muhimu kuhakikisha kuwa utekelezaji wake unafanyika kwa wakati na kwa ufanisi unaoweza kupimika.

Baraza pia linaona kuwa Mpango Biashara umeainisha viashiria vya utendaji (Key Performance Indicators – KPIs) na viwango vya huduma (Overall Minimum Service Standards na Guaranteed Service Standards) ambavyo hutumika na EWURA kutathmini utendaji wa mamlaka za maji nchini. Hivyo, viashiria hivyo vinapaswa kuwa msingi wa kufuatilia utekelezaji wa ahadi zilizotolewa na Kasulu WSSA wakati wa kipindi cha utekelezaji wa Bei mpya (Business Plan, uk. 9–10).

Kwa msingi huo, Baraza linashauri EWURA kuhakikisha kuwa utekelezaji wa tariff utakaoidhinishwa unaambatana na ufuatiliaji wa karibu wa viashiria vya utendaji vilivyoainishwa katika Mpango Biashara. Hususan, EWURA ifuatilie utekelezaji wa malengo ya kupunguza kiwango cha NRW, kuongeza muda na kiwango cha upatikanaji wa huduma za maji, kuboresha ufanisi wa ukusanyaji wa mapato pamoja na kutekeleza miradi ya uwekezaji iliyopangwa. Aidha, Kasulu WSSA iwajibike kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa viashiria hivyo kwa EWURA kwa vipindi vinavyotakiwa ili kuhakikisha kuwa ongezeko la bei linaakisiwa na maboresho halisi ya huduma kwa watumiaji.

11. Baraza linafahamu kuwa lengo la mapitio ya bei si kuongeza mapato ya Mamlaka pekee, bali kuwezesha upatikanaji wa rasilimali zinazohitajika ili kuboresha ubora, uendelevu na upatikanaji wa huduma za maji kwa watumiaji. Hivyo, mafanikio ya tariff yoyote itakayoidhinishwa yanapaswa kupimwa kwa kiwango ambacho Mamlaka itatekeleza ahadi na mipango iliyoainishwa katika Tariff Application na Business Plan,

ikiwemo utekelezaji wa miradi ya maendeleo, kuboresha viashiria vya utendaji na kuongeza ubora wa huduma kwa watumiaji (Business Plan, uk. 17–20 na 53–57).

Baraza linaona kuwa ufuatiliaji wa karibu wa utekelezaji wa viashiria vya utendaji ni nyenzo muhimu ya kuhakikisha kuwa ongezeko la bei linatoa matokeo yaliyokusudiwa. Aidha, ufuatiliaji huo utasaidia kubaini kwa wakati changamoto zinazoweza kujitokeza katika utekelezaji wa miradi, utoaji wa huduma na utekelezaji wa mipango ya biashara, na hivyo kuwezesha hatua stahiki kuchukuliwa kabla changamoto hizo hazijaathiri watumiaji.

Kwa mtazamo wa Baraza, watumiaji wanapokubali kubeba gharama za ongezeko la bei, wanakuwa na matarajio halali ya kuona maboresho ya huduma yakitekelezwa ndani ya muda uliopangwa. Kwa hiyo, ni muhimu kuwepo kwa mfumo madhubuti wa kufuatilia utekelezaji wa ahadi zilizotolewa na Mamlaka pamoja na kutoa mrejesho wa maendeleo kwa EWURA na wadau wengine.

Kwa msingi huo, Baraza linashauri EWURA kuendelea kufuatilia utekelezaji wa viashiria vya utendaji na miradi ya maendeleo iliyoainishwa katika Business Plan na Tariff Application katika kipindi chote cha utekelezaji wa tariff itakayoidhinishwa. Aidha, Kasulu WSSA ihakikishe kuwa taarifa za utekelezaji wa miradi, matumizi ya fedha zinazotokana na tariff pamoja na maendeleo ya viashiria vya utendaji zinawasilishwa kwa EWURA kwa wakati, ili kuwezesha tathmini ya mara kwa mara ya iwapo ongezeko la bei linaendelea kuleta maboresho yaliyokusudiwa katika utoaji wa huduma kwa watumiaji.

12. Baada ya kupitia Maombi ya Mapitio ya Bei za Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ya Kasulu WSSA pamoja na nyaraka zote zilizounga mkono maombi hayo, Baraza linaishauri EWURA kuzingatia yafuatayo wakati wa kufanya uamuzi kuhusu maombi ya tariff:

- i. Kujiridhisha kuwa Kasulu WSSA imewasilisha uchambuzi wa kina wa uwezo wa watumiaji kumudu gharama za huduma (Affordability Analysis) pamoja na

Bill Impact Analysis, ili kubaini athari za tariff inayopendekezwa kwa makundi mbalimbali ya watumiaji.

- ii. Kujiridhisha kuwa kiwango cha tariff kinachopendekezwa kinaungwa mkono na ushahidi wa kutosha kuhusu utayari wa watumiaji kulipia huduma (Willingness to Pay) au uchambuzi mwingine unaolingana na lengo hilo, ili kuhakikisha kuwa tariff inazingatia hali halisi ya watumiaji.
- iii. Kuhakikisha kuwa athari za tariff kwa makundi maalum ya watumiaji zimefanyiwa tathmini ya kutosha, hususan kaya zenye kipato cha chini, watumiaji wa Public Water Kiosks, shule, vituo vya kutolea huduma za afya na makundi mengine yaliyo katika mazingira magumu.
- iv. Kufanya tathmini ya kina ya makadirio ya gharama za uendeshaji (Operating Expenditure – OPEX) na Revenue Requirement, ili kuhakikisha kuwa gharama zote zinazoruhusiwa kurejeshwa kupitia tariff ni za lazima, zina ufanisi na zinaendana na viwango vya utendaji vinavyotarajiwa.
- v. Kujiridhisha kuwa gharama za uwekezaji zinazofadhiliwa na Serikali au Washirika wa Maendeleo hazijajumuishwa katika msingi wa kukokotoa mapato yanayorejeshwa kupitia tariff, ili kuepusha watumiaji kulipia gharama zilezile zaidi ya mara moja (double recovery).
- vi. Kujiridhisha kuwa makadirio ya mapato, ongezeko la wateja, kiasi cha maji kitakachouzwa na viwango vya ukusanyaji wa mapato vina uhalisia na vinaungwa mkono na ushahidi wa kutosha, kabla ya kuidhinisha tariff inayopendekezwa.
- vii. Kuhakikisha kuwa viwango vya huduma (Service Standards) na viashiria muhimu vya utendaji (Key Performance Indicators – KPIs) vilivyoainishwa katika Mpango wa Biashara vinafuatiliwa ipasavyo, ili watumiaji wanufaike na maboresho yaliyoahidiwa katika kipindi chote cha utekelezaji wa tariff.

viii. Kujiridhisha kuwa taarifa zote za kifedha, kiufundi na kiutendaji zinazowasilishwa katika Tariff Application, Business Plan na nyaraka nyingine zinazounga mkono maombi zinaoana, na kwamba tofauti zozote zilizobainika zimefafanuliwa ipasavyo kabla ya kufanya uamuzi wa mwisho.

ix. Kuendelea kufuatilia utekelezaji wa masharti yote yatakayowekwa katika Tariff Order, ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa ahadi zilizotolewa kwa watumiaji na uwasilishaji wa taarifa za utekelezaji kwa wakati.

13. Baraza limelitathmini ombi la Mamlaka (Kasulu WSSA) la mapitio ya bei za huduma za maji kwa kuzingatia Maombi ya Bei, Mpango wa Biashara wa kipindi cha mwaka 2026/27 hadi 2030/31, taarifa za fedha zilizokaguliwa pamoja na nyaraka nyingine zilizowasilishwa kuunga mkono maombi hayo.

Baraza linaona kuwa Kasulu WSSA ina dhamira ya kuboresha utoaji wa huduma za maji kupitia utekelezaji wa miradi ya maendeleo, upanuzi wa miundombinu, kuboresha ufanisi wa uendeshaji na kuimarisha huduma kwa wateja. Aidha, Baraza linafahamu kuwa utekelezaji wa mipango hiyo unahitaji upatikanaji wa rasilimali za kutosha ili kuhakikisha huduma za maji zinakuwa endelevu na zinakidhi mahitaji ya wananchi.

Hata hivyo, Baraza linaona kuwa maombi ya mapitio ya bei yanapaswa kuambatana na uhakiki wa kina wa gharama zinazopendekezwa kurejeshwa kupitia tariff, uhalisia wa makadirio ya mapato, uzingatiaji wa uwezo wa watumiaji kumudu gharama za huduma pamoja na uwepo wa mifumo madhubuti ya kuhakikisha kuwa ongezeko lolote la bei linaakisiwa na maboresho yanayoonekana katika ubora, upatikanaji na uendelevu wa huduma.

Baraza linaunga mkono jitihada za Kasulu WSSA za kuboresha huduma za maji, **lakini** linaishauri EWURA kuhakikisha kuwa uamuzi wowote utakaofanywa kuhusu maombi haya unalinda kwa uwiano maslahi ya watumiaji wa huduma za maji na

uendelevu wa utoaji wa huduma kwa mujibu wa Sheria ya EWURA na kanuni zinazosimamia mapitio ya bei.